



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE



Kumb. Na.LW/DC/IE.40/10 VOL III/38

26/07/2022

**TANGAZO LA KUITWA KWENYE MAFUNZO YA KAZI ZA MUDA ZA
SENSA YA WATU NA MAKAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale anawatangazia waombaji wote wa kazi ya muda ya **Karani wa Sensa, Msimamizi wa Maudhui** na **Msimamizi wa TEHAMA** waliofaulu usaili, kuhudhuria kwenye Mafunzo yatakayoanza tarehe **29/07/2022** katika **Ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Kutwa ya Liwale (Liwale Day Secondary School)** Saa 1.30 Asubuhi.

Waombaji wa nafasi zote waliochaguliwa wanatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

1. Kila mwombaji anatakiwa kufika na **vyeti halisi (Original)** vya kidato cha **IV na VI** na vya mafunzo na ujuzi kulingana na nafasi aliyomba na cheti cha kuzaliwa, bila kusahau kitambulusho cha **NIDA/ namba ya NIDA**.
2. Wasailiwa ambao hawajaona majina yao hawajafanikiwa, hivyo wanashauriwa kuomba tena wakati mwingine.
3. Aidha, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri inawajulisha kuwa hakuna gharama yoyote inayotozwa ili kushiriki mafunzo hayo, hivyo **mnatahadharishwa kujihadhari na utapeli** unaoweza kutokea au kupewa maelekezo mengine yasiyohusiana na mafunzo hayo.
4. Orodha ya majina ya waombaji waliochaguliwa kwa ajili ya mafunzo imeambatanishwa hapa chini na pia inapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Liwale <https://liwaledc.go.tz>

DAMAS M.MUMWI
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
LIWALE

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA
LIWALE



Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne, Agosti 23, 2022